

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

KIKAO CHA THELATHINI NA TATU

21 MEI, 2018



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA THELATHINI NA TATU – TAREHE 21 MEI, 2018

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Taarifa ya mwaka ya Shughuli za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa Mwaka 2016/2017 (*A report of the Activities of the Open University of Tanzania for the year 2016/2017*).

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

277. MHESHIMIWA DKT. RASHID MOHAMED CHUACHUA (MASASI):

- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi
- ya Rais (TAMISEMI):- Jimbo la Masasi lina Shule moja tu ya Sekondari kwa kiwango cha Kidato cha Tano na Sita ambayo ni Sekondari ya Wasichana Masasi nayo imekuwa haitoshelezi kutokana na ongezeko la Wanafunzi wanaofaulu:-

- (a) Je, ni lini Serikali itazipandisha hadhi Shule za Sekondari za Mwenge Mtapika na Anna Abdallah ili ziweze kupokea Wanafunzi wa Kidato cha Tano na Sita;

(b) Je, ni lini Serikali itaajiri Walimu katika Jimbo la Masasi ikiwa ikama ya Walimu wa Sayansi katika Shule za Sekondari 9 zilizopo ni Walimu 84 lakini waliopo ni 24 tu.

278. MHESHIMIWA DKT. DALALY PETER KAFUMU (IGUNGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Mwaka 2015 Serikali ilianzisha Mamlaka ya Mji Mdogo wa Igunga kwa lengo la kusogeza karibu huduma kwa Wananchi na kuleta maendeleo lakini tangu wakati huo hadi leo hii Mamlaka hiyo haijapatiwa fedha za kujiendesha na kutoa huduma kwa Wananchi:-

- (a) Je, ni lini Mamlaka hiyo itatengewa bajeti ili iweze kujiendesha na kufanya kazi zake kwa ufanisi;
- (b) Je, ni lini Mamlaka hiyo itapatiwa fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya Mji huo na kujenga Barabara za lami kilometa 4 zilizokuwa zimeahidiwa na Mhe. Rais wakati wa Kampeni za Uchaguzi za mwaka 2015.

279. MHESHIMIWA REHEMA JUMA MIGILLA

(VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kwa nini Serikali haitaki kujenga Hospitali ya Wilaya ya Tabora Mjini baada ya Hospitali ya Wilaya kupewa hadhi ya Hospitali ya Rufaa.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

280. MHESHIMIWA SUZANA CHOGISASI MGONOKULIMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Lengo la Serikali ni kuingiza fedha zote za Kodi kwenye mfuko mmoja na baadaye asilimia fulani ya fedha hizo zirudishwe kwenye Halmashauri:-

Je, kwa nini isitungwe Sheria ya kuibana Serikali ikiwa haitarejesha fedha hizo kwenye Miji, Halmashauri, Manispaa na Majiji.

WIZARA YA KILIMO:

281. MHESHIMIWA BALOZI ADADI MOHAMED RAJAB (MUHEZA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:- Zao la Katani linalimwa kwa wingi Mkoani Tanga hususan Wilaya ya Muheza na ni zao tegemeo la Uchumi Mkoani humo, na bei ya zao hili katika Soko la Dunia imeongezeka sana:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza ulimaji wa zao hilo Wilayani Muheza;

(b) Je, kwa nini Serikali isitafute mwekezaji mkubwa wa kuwekeza katika Kilimo hicho.

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

282. MHESHIMIWA RASHID AJALI AKBAR (NEWALA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuliendeleza Bonde la Mto Ruvuma ili lilete tija kwa Wananchi hasa Wakulima.

**WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO
WA AFRIKA MASHARIKI:**

**283. MHESHIMIWA MARIA NDILLA KANGOYE
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-
Kumekuwa na malalamiko mengi juu ya matukio ya kikatili dhidi ya Watanzania wanaosafirishwa nje ya nchi na kufanyishwa kazi zisizo rasmi:-

- Je, Serikali imechukua hatua gani kudhibiti changamoto hii.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

**284. MHESHIMIWA MWANTAKAJE HAJI JUMA
(BUBUBU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

- (a) Je, ni lini Serikali itawapatia mtaji wa kuwawezesha kiuchumi Wananchi wengi ambao wamejiunga katika Vikundi vya Uvuvi;

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia vifaa vya kisasa ili kuondokana na vifaa haramu.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

285. MHESHIMIWA SAED AHMED KUBENEA (UBUNGO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Serikali katika Bunge la 10 iliwasilisha Muswada wa Sheria ya Makosa ya Mtandao ambayo ilidhihirika kuwa na upungufu na baadhi ya Wadau waliona kuwa kama Sheria ikipita inaweza kuifanya Nchi kuwa adui wa matumizi ya Mtandao wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na Sheria hiyo sasa inawaathiri Watumiaji wa mitandao, kompyuta, simu za mikononi, saa, television na vifaa vingine vinavyofanana na hivyo:-

Je, ni lini Serikali italeta Bungeni Muswada wa kuifanyia Marekebisho Sheria hiyo inayobana uhuru wa Mwananchi wa kupata habari.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

286. MHESHIMIWA MARIAM NASSOR KISANGI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Tatizo la ada kwa Wanafunzi katika Shule binafsi nchini linazidi kuongezeka siku hadi siku. Mwanafunzi wa darasa la kawaida katika baadhi ya Shule analipa mpaka milioni tatu hali inayosababisha Wazazi wengine kuwapeleka Watoto wao katika nchi jirani za Kenya na Uganda ili kutafuta nafuu ya ada:-

Je, kwa nini Serikali isikae na Wadau husika ili kupanga ada elekezi kwa wenye Shule binafsi.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**DODOMA
21 MEI, 2018**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**